Makanisa Saba Ya Asia

na

J. D. Logan

Makanisa Saba Ya Asia

na

J. D. Logan

Novemba 12, 2011

Makanisa Saba Ya Asia

Ufunuo uliandikwa wakati wa mwisho wa karne ya kwanza ikifuatiwa na kuzaliwa kwa Yesu. Kulikuwa na makanisa ya Wakristo yaliyoanzishwa katika Rumi yote na (katika ulimwengu mwingine). Hataivyo, Kristo alihusika na makanisa saba yaliyoonyeshwa katika kitabu hiki.

Haya yalikuwa ni matunda ya uinjilisti uliofanywa na Paulo na watenda kazi wenzake katika safari yao katika Asia ndogo. Leo, makusanyiko haya yangeweza kuwa katika nchi ya kisasa ambayo ni Uturuki.

Tunapaswa kukumbuka kwamba ujumbe unaelekezwa kwa "malaika" (pengine viongozi) wa kila kusanyiko. Hii ni sawa na jinsi Paulo alivyoagiza, kama ilvyowekwa katika Matendo. 20:28-30. Wazee walipaswa kuwa "waangalizi" (wachungaji) wa kundi. Ilikuwa ni jukumu lao la "kulilisha kundi"; hivyo ilikuwa ni wao ndio Kristo alikuwa akiwaongele. "*…itume kwa makanisa saba yaliyoko katika Asia…*" (Ufu. 1:11).

Kumbuka pia kwamba kama kuna kitu cho chote iliyosifiwa kuhusu kusanyiko, ameonyesha hilo kwanza.

Efeso

Efeso ilikuwa ikiendelea vizuri kimaandiko, lakini "*…kwa sababu umeuacha upendo wako wa kwanza.* (Ufu. 2:4). Haionyeshwi hapa kuhusiana na mafundisho ya uongo, ukengeufu, au maisha ya kidunia, bali njia ya Yesu, "*…ulikoanguka…*" (Ufu. 2:5). Kutoka katika nini?

Walianguka kwa kuacha upendo wao wa kwanza. Shauku yao (ilionekana kwanza walipoongoka) ilitoa njia tofauti na kukosa shauku ambayo ni muhimu kwa kuwa Mkristo wa kweli. Hawana tena "*…njaa na kiu ya haki…*" (Mt. 5:6).

Walikuwa katika hatari ya kuwa vuguvugu, hali iliyoongelewa katika hotuba baadaye.

Kwa kuruhusu upendo wao wa kwanza kupoa, shauku yao kupepea, waliacha upendo wao wa kwanza na lazima watubu au wapoteze "mshumaa wao".

Kumbuka Mt. 5:14-16, "*Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu yam lima. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani. Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.*"

Pia, hii inaendana na maonyo ya Bwana katika Mt. 5:13, "*Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini chumvi ikiwa imeharibika itatiwa nini hata ikolee? Haifai tena kabisa, ila hutupwa nje na kukanyagwa na watu.*"

Efeso walikuwa tena hawawezi "*kufikiria*" mazingira yao kwa sababu walikuwa hawana tena "*hazina*". Pengine ilikuwa vigumu kuwatambua kama Wakristo kwa mfumo wao wa maisha.

Smyrna

Smyrna walikuwa maskini sana katika ulimwengu huu, lakini matajiri mbele za Mungu (Ufu. 2:9). Inaonekana kwamba walikuwa katika sehemu ambayo kulikuwa na pingamizi katika kazi ya Bwana. Tayari walishakumbana na "*mateso*" na niwazi kwamba wangeweza kukumbana nayo zaidi (msitari 10).

Wengine wangeweza "*kufungwa na kujaribiwa*".

Kimsingi kulikuwa na nafasi ndogo ya kuutangaza ufalme kwenye sehemu hii, kutokana na pingamizi, lakini walitiwa moyo kwamba "*wawe waaminifu hata kufa*". Changamoto hii inaonekana kuwatia moyo hadi watakapotoka duniani, au hata kufikia mateso, kuuawa.

Kwa kiwango hiki tunaweza kukumbuka ujuzi wa Petro na Yohana kama ilivyoandikwa katika Mdo. 4:19-20. Walishikiliwa mbele ya wakuu wa Kiyunani kwa sababu ya muujiza wa kuponya katika jina la Yesu. Waliamriwa "*..wasiongee tena au kufundisha kwa jina la Yesu.*" (Msitari 18). Jibu lao lilikuwa ni "*… kwamba ni haki mbele za Mungu kuwasikiliza ninyi kuliko Mungu, hukumuni ninyi wenyewe. Maana sisi hatuwezi kuacha kuyanena mambo tuliyoyaona na kuyasikia.*"

Pergamo

Pergamo waliishi katika sehemu *dhaifu* lakini hawakukana uaminifu wao kwa Mungu na Kristo wake. Hataivyo, walishikilia mambo mawili ambayo haikukubaliwa machoni pa Mungu.

Walishikilia "*Mafundisho ya Wanikolai*" , hatujaonyeshwa sehemu nyingine, isipokuwa Bwana aliuchukia. Ilivyokuwa hatujaonyeshwa kiundani zaidi katika maandiko.

Walishikilia "*Mafundisho ya Balaam*", kuna mengi zaidi. Tofauti na kujisifu kwa kupata faida ya kidunia, alimshauri Balaki kuwajaribu wana wa Israeli, hapo kuhusika katika kuweka ukwazo mbele yao.

Waabudu sanamu hawa wakawa marafiki na Israeli, wakiwaalika katika sherehe zao na ibada, wakijichanganya nao. Hivyo, Israeli

walianguka kwa wakati huu kwa sababu ya mafundisho ya uongo na tabia ya kidunia.

Mungu tayari alikuwa ameshawaonya Waisraeli kufanya hivi. "*…msitaje majina ya miungu mingine, au kusikika kutoka katika kinywa chako.*" (Kut. 23:13). "*…nawe utawapiga wakati huo ndio uwaondoe kabisa, usifanye agano nao wala kuwa hurumia; wala usioane nao;*" (Kum. 7:2).

Kwa njia iyo hiyo, ametuamuru "*Tusipende dunia, na vitu vilivyomo katika dunia…*" (1 Yoh. 2:15).

Pia, "*…ye yote atakayekuwa rafiki wa dunia ni adui wa Mungu.*" (Yak. 4:4).

Tunasoma katika Hesabu 25:1-3 kwa Waisraeli waliamua kuweka makazi yao karibu na Wamoabu na kushiriki katika uzinzi pamoja nao. Kwa sababu yah ii, Mungu hakupendezwa sana. Sio tu kwamba walifanya uzinzi na wale ambao hawakujua ukweli, kinyume na maagizo ya Mungu, bali pia walitenda matendo ambayo hayawezi kuzungumzwa pamoja nao, na hivyo kusababisha ghadhabu ya Mungu. Kwa ajili ya hili, walilipa zawadi mbaya.

Hivyo, "*mafundisho ya Balaamu*" ni, tunajifunza, sio tu ni kinyume na sheria kuwa tariri wa vitu vya dunia, bali pia kufundisha na kuwajaribu watu wa Mungu na dunia na ibada ambayo sio ya kweli.

Pia tunajifunza katika 2 Pet. 2:13-15 kwamba wale wanaoshikilia "*mafundisho ya Balaamu*" ni "*…wamekuwa ni mawaa na aibu…wafanyapo karamu pamoja nanyi;…*".

Pergamo ilihukumiwa kwa kuruhusu hili kuendela kati yao. Yuda :11 inatufundisha kwamba hawa "*…wamekwenda katika njia ya Kaini* (unamkumbuka?) *na kuangamia katika maasi ya Kora.*"

Pergamo, inaonekana haikuwa mfano mzuri kwa kusanyiko lo lote kufuata.

Thiatira

Thiatira ilikuwa mwema, wapole, kanisa lililofanya kazi. Dhahiri ilionekana inaendelea katika kutenda kazi. Hataivyo, walikuwa mshirika wa kike, Yezebeli, aliyejiita nabii aliyekuwa akifundisha na kuwaongoza vibaya baadhi ya washiki wa kanisa kutoka katika uaminifu wao. Baadhi ya washirika hawakuchukuliana na mafundisho yake na hawakujua "*kina cha Shetani*", kama alivyofundisha. (Tunajua "*kina cha shetani*" kiasi kwamba tunaruhusu na kumtumikia.)

Bwana alikiita kile alichokuwa anafanya "*uzinzi*". Alicho maanisha kwa kusema hivi ni "uzinzi" wa kiroho. Wakati, katika ndoa, mtu

mwingine zaidi ya mwenza wa mwingine kisheria analetwa katika uhusiano huo, inaanzisha uzinzi. Hivyo tu, mtu anapomleta mwingine, tofauti na Kristo katika uhusiano huu wa kipekee, hivyo inakuwa imechafuliwa, na hivyo kuanzisha "uzinzi".

Kumbuka: Kuna baadhi ambao hawakubaliani na maelezo haya, wakitazama musitari wa 20, "*… kufundisha na kuwapotosha watumishi wangu kutenda uzinzi, na kula vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu.*" Kimsingi hii insweza kuwa kweli. Hataivyo, haitabadili maana, isipokuwa kubadili kutoka katika neno halisi hadi katika sitiari.

Kiushahidi, sio wote waliojihusisha katika matendo haya ya dhambi pamoja naye (mustari 24). Kwa wao, Yesu aliwaonya (mistari 24-25, "*…sitaweka mzigo mwingine juu yako. Lakini kile ulicho nacho kishikilie hata nitakapokuja.*"

Inaonekana kwamba dhambi ya Yezebeli na wafuasi wake "*hawakuwa na mafundisho haya*". Kristo hakuwambia kuacha kusanyiko, bali afadhali aliwaambia "*Kushikilia sana hata nitakapokuja*".

Sardi

Sardi kama kusanyiko lilikuwa katika mwonekano wa huzuni. Lilikuwa na "*jina lililoishi, lakini lilikufa*". Siwezi kuacha kugundua lawama kutoka kwa Kristo kwa ajili ya dhambi inayojulikana, lakini inaonekana walikuwa wamekufa kiroho. Wao, kama kusanyiko, walikuwa sio vuguvugu, bali walikuwa baridi. Hivyo basi, haitakuwa kosa kuliongelea hili kama ni dhambi.

Tabia yao (jina) wengi wangeweza kuamini kwamba walikuwa hai, lakini, kiukweli walikuwa wamekufa.

Kristo aliwaonya kwamba "*shikilia sana, na ukatubu*".

Inaonekana kwamba kitu kidogo kilikuwa kikiwazunguka katika idadi yao na Yesu hakulitaka life. "*Lakini unayo majina machache katika Sardi, watu wasioyatia mavazi yao uchafu. Nao watakwenda pamoja nami hali wamevaa mavazi meupe, kwa kuwa wamestahili.*" (Ufu. 3:4).

Tena, hakuwaagiza waaminifu kuondoka; zaidi sana "*Kushikilia sana*".

Filadelfia

Hili ni swala la kusanyiko lililo didimizwa na watu waliojiingiza waliodai kwamba wao ni Wayahudi, lakini hawakuwa. Hii ingeweza kuwa na faida gani kwao haijawekwa wazi. Inawezekana kwamba hali hii ili kuwa inafanana na hali ya kanisa la Antiokia, ambapo baadhi ya

wanafunzi kutoka katika kanisa la Yerusalemu walikuwa wanasisitiza kwamba Mataifa "*…lazima watahiriwe na kuitunza sheria…*" (Mdo. 15:24).

Kwa hali yo yote walikuwa waongo, na Bwana hakupendezwa na hilo. Aliwapa nafasi ya kuendelea mbele na kazi yake: "*… nimefungua mlango kwa ajili yako, na hakuna awezaye kuufunga…*". (Ufu. 3:8). Walikuwa na "*nguvu kidogo*". Walipaswa kuchukua hatua ya huu mlango uliofunguliwa; kuendeleza kazi yao njema.

Hii inaonekana kuwa hali ya makusanyiko mengi leo, na inapaswa kuwa mfano mzuri kwa wote.

Laodikia

Kama jinsi ilivyo kwa katika kila kusanyiko iliyotajwa, Laodikia haikuwa katika moto wa shauku ya "*upendo wa Kwanza*", ama walikuwa wameganda kama barafu, kama jinsi ilivyokuwa kwa mengine. Inaonekana kwamba kwa kiasi fulani "walikuwa vuguvugu". Hii, inaonekana kwamba walikuwa hawaja mwonja Bwana, na hivyo alijiandaa kuwatema (tapika) watoke katika kinywa chake (Mustari 16).

Baadhi ya viakula vinakuwa na ladha viwapo moto na vingine vinapendwa kuliwa vikiwa na ubaridi. Pia vinapendeza kuliwa vikiwa na uvuguvugu. Kufuatilia hili zaidi, inaonekana kwamba walikuwa na maisha ya Kikristo kwa kila upande. Kama ilivyo kwa makanisa mengi leo, wangeweza kukubali mafundisho yo yote ambayo hayakuweza kusumbua amani ya akili zao. Walikuwa wameridhika na hawakuitaji zaidi "kusukuma gurudumu".

Walikuwa wameridhika wenyewe katika utajiri na kiburi chao cha msimamo wao katika jamii. Tatizo ni kwamba walimtupa Bwana nje ya kusanyiko lao (msitari 17).

Je hii inaweka kitu katika akili zetu? Je tuwahi kuona makanisa makubwa kama haya? Hii kimsingi SIYO mzuri wa kusanyiko lolote kuweza kulifuata!

Kwa makanisa haya yote, Yesu anawaonya, "*…aliye na sikio na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa…*" alichowaambia ilikuwa ni "*kushikilia sana*", "*tubu*", "*kasha, na uyatie nguvu mambo yaliyo pungua*", na "*ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, ili uweze kuwa tajiri*".

Zawadi ilikuwa kubwa kwa wale wote ambao walisikiliza na kukubali ipasavyo. "*Yeye ashindaye nitampa kula matunda ya mti wa uzima…*", "*…nitampa taji ya uzima…*", "*…nitampa uwezo dhidi ya mataifa*". Ahadi hizi (na mengine mengi) zilihakikishwa kwa "*Yeye ashindaye*".

Kila mmoja wetu anapaswa kujiangalia ndani yake na kujiuliza, “Ni yapi kati ya makanisa haya saba mimi ni mshiriki? Kuna chaguzi saba.

Yesu anasema, “*Tazama nasimama mlangoni, nabisha: kama mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia ndani na kula pamoja naye, nay eye pamoja nami.*” (Ufu. 3:20).

Ndugu yenu katika Bwana,

J.D. Logan